

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA AROBAINI NA SITA



17 JUNI, 2019

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA AROBAINI NA SITA – TAREHE 17 JUNI, 2019

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2019/2020 pamoja na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na Mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2018, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2019/2020 pamoja na Mapendekezo ya

Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

##### **380. MHESHIMIWA OMAR ABDALLAH KIGODA (HANDENI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kuna mgogoro mkubwa wa ardhi unaondelea katika Wilaya ya Handeni ambao kama hatua za haraka hazikuchuliwa unaweza kusababisha ugomvi mkubwa kati ya Wananchi:-

Je, nini tamko la Serikali katika kuzuia tatizo hilo.

#### **WIZARA YA MAJI:**

##### **381. MHESHIMIWA JUMA SELEMANI NKAMIA (CHEMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Wananchi wa Vijiji vya Mombose na Bubutole watakaopisha ujenzi wa Bwawa la Farkwa watalipwa fidia.

## **382. MHESHIMIWA ALBERT OBAMA NTABALIBA (BUHIGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itavipatia maji Vijiji vya Rusaba, Kitelema, Migongo, Nyamboza na Kibwigwa.

## **WIZARA YA NISHATI:**

## **383. MHESHIMIWA TIMOTHEO PAUL MNZAVA (KOROGWE VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Wa Nishati:- Katika Jimbo la Korogwe Vijijini bado Vijiji vingi havina umeme:-

Je, ni lini usambazaji wa umeme kupitia REA utakamilika katika Vijiji vya Jimbo la Korogwe Vijijini.

## **WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

## **384. MHESHIMIWA JUMA KOMBO HAMAD (WINGWI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:- Ni muda mrefu sasa Serikali imekuwa kwenye mchakato wa kupata vazi la Taifa:-

- (a) Je, Serikali imefikia hatua gani ya mchakato huo;
- (b) Je, ni lini Watanzania wategemee kuwa na vazi la Taifa.

#### **WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

#### **385. MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Barabara ya Makutano – Sanzate imejengwa kwa muda mrefu:-

- (a) Je, ni lini barabara ya Makutano – Sanzate itakamilika;
- (b) Je, Serikali kupitia Watalaam wake imeridhika na kiwango cha uwekaji lami katika barabara hiyo.

#### **WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

#### **386. MHESHIMIWA FRANK GEORGE MWAKAJOKA (TUNDUMA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, ni lini Serikali itatafuta masoko ya uhakika ya ndani na nje kwa Wakulima wanaozalisha mazao ya chakula kama Mahindi na Mpunga.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

### **387. MHESHIMIWA HAWA SUBIRA MWAIFUNGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Ajali za barabarani bado zimekuwa tishio kubwa kwa maisha ya Watanzania; kutokana na ajali hizo tunapoteza nguvu kazi ya Taifa na familia nyingi zinabaki zikitaabika:-

Je, Serikali imejipanga vipi kukabiliana na ajali hizo.

### **388. MHESHIMIWA ZAINAB ATHUMAN KATIMBA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

(a) Je, Serikali ipo tayari kuwaeleza Watanzania hususan Vijana kuwa ni hatua gani zimechukuliwa na Serikali ya Awamu ya Tano katika kuwabaini, kuwachunguza na hatimaye kuwahukumu wale wote

waliobainika kujihusisha na mtandao wa biashara za Dawa za Kulevya;

- (b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia Vijana walioitumbukia kwenye dimbwi la matumizi ya Dawa za Kulevya;

## **WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

### **389. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA (URAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Katika Wilaya ya Urambo kulikuwa na Chuo cha Ualimu ambacho kilisaidia sana kuleta chachu ya Maendeleo ya Elimu na Uchumi kwa Wananchi wa Urambo:-

- (a) Je, ni sababu zippi zilizosababisha Chuo cha Ualimu Urambo kufungwa/kuhamishwa;
- (b) Je, Serikali haioni iko haja ya kuangalia upya uwezekano wa kurudisha Chuo cha Ualimu Urambo.

## **IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:**

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2019 (*The Finance Bill, 2019*).

## V. HOJA ZA SERIKALI:

### WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba, Bunge likubali kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Kwamba, Bunge likubali kuitisha Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

*(Majadiliano yanaendelea)*

DODOMA  
17 JUNI, 2019

S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE